# Orodha ya Mambo Kadhaa katika Kutokomeza Udhalimu

## The Checklist for Ending Tyranny

**Peter Ackerman and Hardy Merriman**

From the book: 'Is Authoritarianism Staging a Comeback?'
Editors: Mathew Burrows and Maria J. Stephan
The Atlantic Council, Washington D.C. — 2015
Translation: JPD Systems, March 2019

# Orodha ya Mambo Kadhaa katika Kutokomeza Udhalimu

**Na Peter Ackerman na Hardy Merriman**

Migogoro mikubwa zaidi duniani leo si ya kati ya nchi na nchi bali ni ile iliyo ndani ya hizo nchi, ambayo inahusisha wadhalimu dhidi ya watu wanaowakandamiza. Inaaminika kwamba watu hawa wanaonyanyasika wana njia mbili za kuchagua: ama kukubaliana na udhalimu wakiamini kwamba utapungua makali au kuleta uasi kwa njia ya matumizi ya nguvu ili kuleta uhuru. Mtazamo huu unapingwa na ukweli kwamba kampeni za kutumia nguvu ya umma (mara nyingine mavuguvugu ya "nguvu ya umma" au migogoro baridi) zimetokea mara nyingi zaidi kuliko ambavyo inafahamika. Mwanzoni mwa mwaka 1900, kulikuwepo wastani wa kampeni moja kubwa ya matumizi ya nguvu ya umma kumpinga mtawala aliyeko madarakani kwa mwaka.[1] Mavuguvugu haya yanayoongozwa na wananchi yameonesha mara kadhaa matokeo ya migogoro mikubwa ya kijiografia na kisiasa na vipindi vya mpito vya kidemokrasia tangu 1972.[2] Hata hivyo, watunga sera, wanazuoni, waandishi wa habari, na wafuatiliaji wengine wenye mapenzi mema wanaichukulia kawaida tu nguvu ya wananchi wa kawaida kana kwamba haiwezi kupambana na udhalimu na kuleta haki bila kutumia mabavu.

## Uchambuzi Kuhusu Yaliyofichwa Machoni

Maandamano ya Tunisia na Misri mwaka 2011, na hivi karibuni 2014, ni mifano ya namna wananchi wa kawaida wanaweza kuwashangaza watu namna walivyo na nguvu na uwezo wa kufanya mabadiliko. Hakuna aliyeona maandamano haya yakianza, lakini hii inayafanya yaonekane ya kipekee sana. Wachache sana kama wapo waligundua "maandamano ya halaiki" yakitokea Serbia (2000), Georgia (2003), na Ukraine (2004). Milongo michache kabla, hakuna aliyeweza kung'amua kwamba nguvu ya umma iliyopangiliwa kisawasawa ingeweza kupindua utawala wa dikteta wa Ufilipino Ferdinand Marcos (1986), dikteta wa Chile Augusto Pinochet (1988), utawala wa kisovieti nchini Poland (1989), au ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini (1992).

Kadri wataalam wa kikanda na kimataifa wanavyoelezea migogoro hii na



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

mingineyo ya amani, mara nyingi huhitimisha kwamba mifano mingi ya kufanikiwa kwa nguvu ya umma ni mambo ya kushangaza kihistoria kwa kuwa huwa ni mfumo wa mazingira ya kipekee kwenye nchi husika kwa muda pangwa. Kwa kuwa mienendo yake huwa ya kipekee, huwa haitazamwi kama mkakati jumuishi ambao watu wanaweza kuutumia kuwapindua viongozi mbalimbali dhalimu. Hata hivyo, haya mambo yameshakuwa dhahiri machoni pa viongozi dhalimu duniani. Wamegundua kwamba mavuguvugu ya nguvu ya umma ni hatari sana kwa utawala wao wa sasa.

Kutokana na migogoro baridi ambayo imekuwa ikiongezeka tangu mlongo uliopita ni muhimu sana kwa wale wanaounga mkono mabadiliko ya kidemokrasia kuhuisha uelewa wao juu ya kwanini mavuguvu ya nguvu ya umma hufanikiwa. Migogoro baridi hufanikiwa mara nyingi kwa nyakati tofauti tofauti kwa sababu hutumia uhalisia katika maeneo mawili: kwamba tawala za mabavu hutegemea utii wa hali ya juu wa watu wanaonyanyasika ili kuendelea kuwadhibiti, na ya kwamba si kila mtu kwenye tawala za hivyo ni mwaminifu.

## Namna Nguvu ya Umma Inavyofanya Kazi

Kwa kuzingatia ukweli huu katika maeneo hayo mawili, wapinga udhalimu huleta makundi ya watu pamoja na kuhakikisha hawayumbi katika kuweka kando utii wao na hivyo kuweka mashinikizo—kwa kupitia mbinu kama migomo, masusio, maandamano makubwa, na hatua nyingine—kuzimisha mfumo kandamizi na kupata haki zote na uhuru. Ushiriki katika nguvu ya umma unapofanyika kwa mbinu tofauti tofauti na unavyoongezeka, kamatakamata kwa wapinga ukandamizaji huwa ngumu kurudisha amani na utulivu bali badala yake huwa kuna uwezekano zaidi wa mtego wa panya kumgeukia mtegaji.

Kadri shughuli zinavyokatizwa, mipasuko nayo huanza kuonekana ndani ya serikali na taasisi nyingine (yaani polisi, jeshi, vyombo vya habari na kwenye siasa, urasimu na uchumi) ambayo muhimu sana kwa dola. Mipasuko hii mara nyingi husababisha watu kupuuza maagizo kutoka juu, na kadri upuuzaji huu unavyoongezeka, nguvu nyeti ambayo mkandamizaji hutegemea kwa ajili ya utawala wake—udhibiti wa rasilimali vitu, rasilimali watu, maarifa na elimu ya watu, watoa taarifa, na uwezo wa kuweka vikwazo —huathiriwa. Wanapokuwa wameachwa bila safu ya uongozi ya utoaji amri zao, watu dhalimu mwishowe huwa hawana namna zaidi ya kuachia ngazi kutokana na mashinikizo endelevu



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

kutoka kwa umma. Matokeo mara nyingi huwa ni kufanyika kwa mabadiliko.

## Maarifa dhidi ya Mazingira

Kutokana na kuongezeka kwa matukio na athari za nguvu ya umma, ni muhimu kujua nini husababisha matokeo hayo. Je, mazingira kabla ya mgogoro kuanza yanaweza kusaidia kubashiri mshindi atakuwa nani kati ya walio kwenye vuguvugu na mtawala? Au ushindi wa upande wowote unategemeana na mikakati na akili inayotumika kwenye kupambana?

Dhima ya Kituo cha Kimataifa cha Migogoro Baridi (ambacho sisi ni wajumbe wake) ni kuhakikisha kuwa maarifa yanazidi mazingira katika kuangalia hatua na matokeo za vuguvugu. Hili mara nyingi husababisha msukumo mkubwa kwa hasimu kutumia mabavu.

Usemi "Nguvu ya umma hufanya kazi tu pale inapotegemea mahasimu wasio katili sana" ni kibwagizo cha mara kwa mara, lakini watu wanasahau ubaguzi wa rangi ulivyotokomezwa Afrika Kusini, Pinochet kule Chile, Marcos kule Ufilipino, au utawala wa kikomunisti kule Poland. Mifano ya hivi karibuni ni pamoja na Hosni Mubarak wa Misri na Ben Ali wa Tunisia. Hakuna utawala hata mmoja kati ya hizo ambao tunaweza kusema ulikuwa wa kikatili kiasi, au haukuwa tayari kutumia vitisho kupita kiasi.

Mifano hii ya kimaneno zaidi inalandana na uchambuzi wa kiidadi zaidi. Mwaka 2008 shirika la Kutetea Uhuru, yaani Freedom House, lilifanya utafiti kuchunguza sababu mbalimbali za kimuundo na namna inavyoweza kushawishi nguvu ya umma katika vipindi vya mpito 64 kwenye serikali za kiimla kuanzia 1975 hadi 2006. Hii hapa ni nukuu ya hitimisho kuu:

> …katika sababu za kisiasa na za kimazingira zilizofanyiwa utafiti hakuna zilizoonekana kuwa na mashiko kitakwimu kwenye kuleta mafanikio au kushindwa kwa mavuguvugu ya umma ….
> Mavuguvugu ya umma ni rahisi kufanikiwa kwenye nchi zisizoendelea, maskini kiuchumi kama ilivyo kwenye taasisi tajiri.
> Utafiti unaonesha pia kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kwamba tofauti za kikabila au kidini zina athari kubwa kwenye uwezekano wa kuzuka kwa upinzani wa kutosha wa wananchi.
> Pia aina ya utawala inaonekana kutokuwa na ushawishi mkubwa



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

> sana kwa wananchi kwenye kuunga mkono mavuguvugu ya umma.[3]

Sababu pekee iliyoonekana kwenye utafiti ambayo ilikuwa na mashiko kwenye kuzuka kwa mavuguvugu ya nguvu ya umma ilikuwa utawala wa kutoka chini kwenda juu. Watunzi wanasema:

> Utafiti unaonesha kwamba kuna uwezekano mkubwa sana wa utawala wa kutoka chini kwenda juu kushabihiana kwa kiasi kikubwa na kuzuka kwa vuguvugu kubwa la umma kukabiliana na mamlaka ya dola. Kuna uwezekano pia wa kinyume chake: kadri kunapokuwa na ugatuaji wa madaraka ya serikali, ndivyo vuguvugu la kuwakusanya raia pamoja kupambana hupungua.[4]

Hivyo basi, wakati utafiti unavyoelekeza macho yake kupata mazingira ambayo hushawishi mienendo ya mavuguvugu ya umma, matokeo jumuishi yanapinga kwa kiasi kikubwa kwamba mazingira huchangia kutokea kwa migogoro hii.

Miaka mitatu baadaye, kupitia tuzo yao ya ushindi ya kitabu bora cha mwaka 2011, *Kwanini Nguvu ya Umma Hufanikiwa: Mantiki ya kimkakati ya migogoro baridi*, wanazuoni Erica Chenoweth na Maria Stephan walichambua kwa kina kampeni 323 za kutumia nguvu na za amani ambazo zilizisumbua serikali tulivu kati ya mwaka 1900 na 2006.[5] Walichobaini kikubwa ni kwamba kampeni za amani zilifanikiwa kwa 53% dhidi ya za kutumia nguvu ambazo zilionesha 26% ya muda uliotumika.[6] Waligundua pia kwamba wakati kamatakamata ya serikali na sababu nyingine za kimuundo zinaweza kushawishi mafanikio kwenye kampeni za nguvu ya umma (ingawa si sana kama inavyofikiriwa— kwenye dola lenye kutumia kamatakamata kiwango cha mafanikio ni kama 35%), waligundua kwamba hakuna sababu za kimuundo zinazoweza kuwa kisababishi cha vuguvugu.[7] Baada ya kuchambua data kwa kina hitimisho lao ni kwamba "kuna ushahidi wa kutosha kwamba vuguvugu la umma hufanikiwa mara nyingi bila kujali sababu za kimazingira ambazo watu hutumia kuhusisha na kushindwa kwa kampeni za kudai haki kwa amani."[8]

Matokeo haya yanaonesha mazingira yasiyo sahihi ambamo busara za kawaida juu ya nguvu ya umma zimejikita. Maarifa na uchaguzi wa kimkakati huwa muhimu zaidi kuliko mazingira katika kusababisha matokeo ya migogoro hii. Hili si suala la kushangaza hasa tunapoona kwamba maamuzi ya mwanzo ya



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

kimkakati yanafanywa na wapinga udhalimu katika kupigana. Ni sawa kabisa kuamini kwamba, mazingira ya nje yakiwa ndo kiini cha matokeo, hapo uchaguzi wa kimkakati wa namna raia wapambane na udhalimu ni muhimu sana, na kiwango cha mafanikio kati ya kudai haki kwa kutumia nguvu na kule kwa njia ya amani kwa muda fulani na kwa nyakati tofauti kunatakiwa kushabihiana.

Hata hivyo, data hazioneshi hivyo. Kati ya mwaka 1900 na 2006 mavuguvugu mengi ya nguvu ya umma yalifakiwa mara dufu, na mifano ya tafiti za hivi karibuni zinaonesha kwamba utofauti kwenye viwango vya mafanikio haujabadilika sana.[9] Wengine wanaweza kuliangalia hili kwa kusema kwamba raia wapinga uonevu huchagua mapambano ambayo yanaonekana rahisi kushinda, lakini Chenoweth na Stephan waliiona hoja hiyo na kuonesha kwamba "… kampeni nyingi za amani zimeonekana katika tawala za kiimla … ambapo hata upingaji wa serikali kwa njia ya amani unaweza kuwa na mwisho mgumu."[10]

Mshindi wa Tuzo ya Nobeli - mwanauchumi Thomas Schelling alipatia kwenye nsha yake aliyoiandika miaka zaidi ya 50 iliyopita kwenye kitabu chenye jina la *Nguvu ya Umma kama Njia ya Kujilinda Kitaifa: Mapambano bila kuvunja amani dhidi ya udhalimu*. Hili ni hitimisho lake:

> Mdhalimu na watu wake mara kadhaa wanafanana sana kwenye nafasi zao. Wanaweza kumkatalia mengi ambayo anataka yatimie—wanaweza, hii ni pale wanakuwa na umoja katika kukataa kumuunga mkono. Na yeye anaweza kuwanyima yote wanayotaka—anaweza kuwakatalia kwa kutumia mamlaka yake … ni suala la kurumbana pande zote, kama wako makini na wana umoja wanaweza kukataa yale wengine wanataka, na hivyo kusubiria nani atashinda.

Kwa mujibu wa Schelling, mbinu walizoamua kutumia raia walio kwenye mapambano zina gharama na faida, kama ilivyo upande wa mahasimu wao. Mshindi ni yule kinara anayeonesha gharama na faida hizi kwa ufasaha kwa upande wake. Kinara aliyeiva kwenye nguvu ya umma huwaweka sawa watu wasimamishe kazi ili kuongeza upuuzaji wa maagizo kutoka juu, na hupenda kutumia mbinu ambazo kufanya vimgomo baridi vya kazi kuzaa utunishaji misuli zaidi. Mtawala makini hutaka kuwe na utii wa sheria bila shuruti, na mara nyingi hutumia mabavu, na mara chache hupenda atumie nguvu kidogo tu kuleta utii wa hali ya juu. Hali ya kugomea maagizo ya mkubwa inapozidi ile ya utiii inaonesha wazi nani mshindi.



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

## Orodha ya Mambo Kadhaa

Ikiwa maarifa na uchaguzi wa kimkakati ni mambo muhimu katika kushawishi matokeo ya mavuguvugu ya nguvu ya umma, basi tunaweza kuainisha uwezo wa kupambana kwa pamoja, maarifa, na chaguzi kwenye mavuguvugu mengi ambayo yanaonesha vigezo vya mfanano vya mafanikio. Mambo kadhaa chachu yanayohusu mavuguvugu yanaweza kuchambuliwa, lakini makuu matatu ni:

1. Uwezo wa kuwakutanisha raia
2. Kupanga mipango ya utekelezaji
3. Maandamano ya amani

Mambo haya yanapokuwepo kwenye vuguvugu la nguvu ya umma, huruhusu mienendo mikuu mitatu ya wazi yenye nguvu ya kulifanya vuguvugu kufanikiwa. Mienendo hii ni:

1. Ongezeko la raia kwenye matumizi ya nguvu ya umma
2. Kamatakamata kupungua, na kugeuziana kibao kuongezeka
3. Ongezeko la watu kupuuza maagizo kutoka juu

Kwa kuyachukulia kwa pamoja, mambo haya chachu matatu na mienendo mitatu ndo tunaita "Orodha ya mambo kadhaa." Tunaamini kwamba kwa kupata mambo haya chachu na mienendo hii kunaongeza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa vuguvugu kufanikiwa. Kwa mantiki hii, orodha ya mambo kadhaa siyo kanuni yenye kuhakikisha kuna matokeo, bali ni mfumo unaosaidia watu kuweka mawazo yao sawa na kuongeza ufanisi.

Katika kufanikisha hili, kazi moja ya orodha ya mambo kadhaa ni kuhakikisha vipangamizi vinavyoweza kujitokeza kwenye mgogoro vinapotea. Utata ni moja ya changamoto kubwa zaidi wanazokumbana nazo waandamanaji, na ni ngumu kung'amua sababu ambazo ni muhimu zaidi kwenye kufanya maamuzi katika mgogoro. Tunahitimisha kwamba, kama manaharakati au jumuiya ya kimataifa inataka kufanya uchambuzi wa hatima ya vuguvugu, kuulizia kama mambo haya chachu matatu na mienendo mitatu kwenye orodha ya mambo kadhaa ipo itasaidia kama msingi wa uchambuzi wa hali halisi ya vuguvugu, mafanikio, kushindwa kwake, na hatima ya ushindi.

Ngoja tudadavue orodha hii ya mambo kadhaa hapa chini:



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

**1. Uwezo wa kuwakutanisha raia**

Watawala wana werevu mkubwa katika kuwagawa watu na wale walio tayari kupambana nao lazima wawe werevu zaidi katika kuleta umoja. Kuleta umoja na kuhakikisha unadumu si kazi ndogo, lakini kikuu katika kufanya hivyo ni kuwa na maono ya pamoja na jumuishi kwa ajili ya vuguvugu la nguvu ya umma. Katika kufanikisha hili, lazima vinara wa vuguvugu wawe na elimu ya kina inayohusu manung'uniko, mategemeo, mila, na thamani ya makundi mbalimbali ya jamii ambayo wanataka kuyaleta pamoja. Elimu hii huwa ni msingi wa kuweka na kuwasilisha maono ambayo yanavutia uungaji mkono wa wengi na kuwaleta wengi pamoja. Maono thabiti huendana na uzoefu na mawazo binafsi ya wananchi wa kawaida na kuwaleta pamoja katika kutumia nguvu ya umma kama kundi.

Kipengele kingine muhimu cha kujenga umoja ni uwepo wa viongozi na muundo wa uongozi ulio halali. Kushiriki kwenye mavuguvugu ni hiari ya mtu, na viongozi kwenye kuwaleta wananchi pamoja hawapaswi kuwalazimisha wala kuwadhibiti. Hii ina maana maamuzi katika vuguvugu yanapaswa kukuendeshwa kwa njia ambazo zitaonekana halali mbele ya macho ya raia wanaoombwa kuungana kudai haki. Kila vuguvugu huwa na njia yake katika kufanikisha hili—wengine hufuata ngazi, wengine kwa njia ya ugatuaji, na wengine kwa njia mseto kwa muda mrefu. Pamoja na uwepo wa uongozi na muundo madhubuti kwenye vuguvugu, kuna aina mbalimbali za uongozi katika mavuguvu, na umoja ndo kiungo muhimu katika kuwaleta pamoja. Kwa kila kiongozi wa kitaifa mwenye talanta, kuna viongozi wengine wa ngazi za chini ambao wanatakiwa wawe werevu sana katika kuleta ushirikiano, maridhiano, na nia ya pamoja miongoni mwa makundi tofauti tofauti. Ni wajibu wa viongozi tofauti tofauti, kwa ngazi tofauti tofauti (za chini na za kitaifa), kutoka pande zote za nchi, wenye kuwakilisha maslahi ya makundi tofauti tofauti, kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuendeleza umoja kwa muda mrefu.

Tuna ushahidi wa mambo haya mawili yahusuyo umoja katika nguvu ya umma yalivyotumika katika vuguvugu la kupinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini miaka ya 1980. Mamia ya makundi ya raia nchini humo yalizuka kipindi cha mlongo huo kudai mahitaji muhimu kama maji safi na huduma, wakati huo huo wakiungana kwa mtazamo mmoja wa kutokomeza ubaguzi wa rangi na kupata mwafaka wa kitaifa. Makundi haya ya raia ambayo yaliungana na chama cha United Democratic Front, yalikuwa na viongozi wa ngazi za chini ambao waliweza kuongoza kwa ufanisi kwa kutumia mbinu za wananchi wa kawaida (kama kususia kununua

bidhaa) kwa mambo mbalimbali maeneo hayo, wakati huo huo wakiwasiliana na kushirikiana na uongozi wa vuguvugu wa ngazi ya taifa.

**2. Kupanga mipango ya utekelezaji**

Kuingia miguu yote kwenye kutumia nguvu ya umma ni kazi ngumu kuliko ambavyo wengi hufikiri. Picha inayokuja kichwani watu wanapowaza juu ya nguvu ya umma ni mgomo, wakati hiyo ni mbinu moja tu kati ya mamia. Mavuguvugu yaliyofanikiwa yanajua mbinu ipi itumike, lini, wapi, kivipi, na nani, na ilengwe kwa nani, na ifuatiwe na mbinu gani nyingine.

Katika kujibu maswali haya kwa ufasaha, kunahitajika kupanga mipando kwa kuzingatia uchambuzi wa kina juu ya uwezo, udhaifu, fursa, na vitisho vya hasimu, lakini pia tathmini ya mazingira ya mgogoro na watazamaji wa nje (ikiwa ni pamoja na jumuiya ya kimataifa) ambao wanaweza kuhamasisha mgogoro. Kutokana na taarifa hii, mavuguvugu yanaweza kuweka malengo ya muda mfupi, wa kati na mrefu na mipango ya namna ya kutekeleza hayo malengo. Wakati mipango hiyo inabadilika kadri muda uendavyo kwa kutegemeana na matukio yaliyopo (kama ilivyo kwenye mipango), mchakato wa kupanga mipango na mtazamo ni muhimu zaidi kwa washiriki wa vuguvugu kuliko mpango wenyewe mahususi.

Kwa haraka haraka, tunaona wazi kabisa muingiliano wa maarifa na mazingira katika mgogoro wakati wa kupanga mipango ya utekelezaji. Msingi wa kupanga mipango ya utekelezaji ni tathmini ya mazingira— rafiki na ambayo siyo rafiki— ya vuguvugu. Vuguvugu hupanga kutumia mazingira rafiki na kushinda, kufanya mabadiliko, au kukwepa mazingira ya kipinzani kwa kutumia maarifa na uchaguzi wa kimkakati.

Mfano hai wa upangaji mipango ya utekelezaji unaonekana kwenye vuguvugu la Solidary (Mshikamano) nchini Poland miaka ya 1980. Kwa kutambua uwezo wao, wafanyakazi waliweka madai ya dhati yenye uhalisia na yenye mlengo wa kisiasa kupitia vyama huru vya wafanyakazi (lakini walijihami na kile kilichoitwa lengo hafifu la kuuzimisha utawala wa kikomunisti); wakawekeza nguvu zao kwenye kuwaunganisha wafanyakazi na mshikamano baina ya wafanyakazi mbalimbali dhidi ya uwezo wa kiuchumi wa hasimu wao na ukosefu wa uhalali; na wakachagua kufanya mgomo makazini kama mbinu sahihi (badala ya kuingia barabarani nje ya maeneo yao ya kazi, kitu kilichowaletea kamatakamata walipojaribu kipindi fulani cha nyuma). Hii iliongezewa nguvu na wafanyakazi waliojiegemeza kwenye taasisi mbadala— hasa magazeti na majarida huru— ambayo yalikuwa yameshaandaliwa kwa zaidi ya mlongo ili kurahisisha



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

© 2014 Peter Ackerman na Hardy Merriman
mawasiliano kwenye miji. Kwa kuchagua lengo la kimkakati, mlengwa sahihi, na mbinu sahihi (mgomo kazini na kutumia taasisi mbadala) ambazo waliweza kuzipata kirahisi, vuguvugu la Solidarity lilifanikiwa kwenye mazingira ya mgogoro, likashinda mazingira ya upinzani, na kufikisha malengo pangwa ya kupata nchi ya Poland yenye demokrasia mnano mwaka 1989.[12]

**3. Maandamano ya amani**

Kukaa kwenye maandamano ya amani — uwezo wa waandamanaji kuendelea kudai haki bila kutumia nguvu hata kama wanachokozwa—ni muhimu sana katika mienendo ya nguvu ya umma. Kwenye maandamano ya amani, mavuguvugu huhakikisha kuna raia wengi wanaoshiriki, huhakikisha hasimu anapata taabu sana kwenye kamatakamata yake, huhakikisha mtego wa panya unamrudia mtegaji, na hata vibaraka wake kupuuza maagizo yake. Kulingana na utafiti wa Chenoweth na Stephan, mambo haya husaidia sana viwango vya mafanikio kati ya kampeni za matumizi ya ubabe na nguvu ya umma.[13]

Katika kufanikisha maandamano ya amani, lazima mavuguvugu yawe na uhakika kwamba nguvu ya umma ni nyenzo katika kumaliza mgogoro. Tarifa juu ya namna nguvu ya umma inavyofanya kazi na historia yake ni msaada tosha kipindi hiki, maana huwa ni mkakati mkubwa wenye kujenga ushindi endelevu kadri muda unavyoenda na kuonesha kwamba kweli nguvu ya umma ni mwarobaini. Mavuguvugu pia huhakikisha kuna maandamano ya amani kwa kuweka utamaduni na miongozo yenye kuhakikisha hilo linatimia. Kwa mfano, vuguvugu la Otpor nchini Serbia lililomng'oa Slobodan Milosevic kwa umakini mkubwa liliwapa mafunzo wajumbe wapya juu ya namna nguvu ya umma inavyofanya kazi, na kwanini ni muhimu siku zote kudai haki kwa njia ya amani.

Jitihada hizo hazitaki vuguvugu ili kufanya hoja za kimaadili juu ya matumizi ya amani muda wote, bali watu lazima wahamasishane kujua faida halisi za maandamano ya amani, huku wakikumbuka mifano kama Syria (kama mfano wa hivi karibuni wa kutia huzuni) ambapo kutokuwa wavumilivu au kukosa kujiamini kwenye nguvu ya umma kulisababisha matumizi ya nguvu kubwa, ambayo ilileta maumivu ya hai ya juu kwa wengi.

**4. Ongezeko la raia kwenye matumizi ya nguvu ya umma**

Watu wengi kushiriki kwenye nguvu ya umma ni kiashiria kikubwa cha mafanikio ya vuguvugu.[14] Hii inaingia akilini kwa sababu kadri watu wanavyokiuka makubaliano na utii kwa mtawala, ndivyo mtawala hupoteza nguvu, na ndivyo humgharimu zaidi akijaribu kudhibiti mambo. Zaidi ya hilo,



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

tunaamini pia kwamba ongezeko la raia katika kushiriki pia huongeza uwezekano wa mtego wa panya kumgeukia mtegaji na kuna ushahidi wa kiidadi kwamba ushiriki wa raia wengi kwenye maandamano husababisha vibaraka wa hasimu kutotii maagizo yake.[15]

Kwa udadavuzi zaidi, umuhimu wa ushiriki wa raia wengi unaonekana kwenye mapinduzi ya 2011 nchini Misri na Tunisia ambayo yalipata uungwaji mkono na makundi mengi tofauti tofauti —wanaume kwa wanawake; wenye dini na wapagani; vijana, umri wa kati,na wazee; wenye vipato vya chini, na vya kati, wakaao mijini na vijijini. Hata hivyo, vuguvugu la wanafunzi la 1989 nchini China na vuguvugu la Kijani la 2009 yalipata ushiriki wa mamilioni ya watu na kugonga vichwa vya habari, lakini hayakufanikisha malengo pangwa kwa sababu hayakuwa na ushiriki wa raia wa kuzidi idadi ya awali ya kidemografia.

Kupata mwamko mkubwa kwenye nguvu ya umma ni matokeo ya mambo chachu matatu ya mwanzo kwenye orodha ya mambo. Maono ya pamoja husaidia kujenga umoja na kuwa na sauti moja. Kupanga mipango ya utekelezaji huleta kujiamini na mbinu nyingi za kusaidia watu wawe wavumilivu kwa lolote, watumie muda uliopo, na kujitoa mhanga kupambana. Mkakati sahihi huwa na mbinu mbadala kwa ajili ya maskini, matajiri, vijana, wazee, na kila mtu ili radi tu awe na cha kufanya, kidogo au kikubwa, ili kuunga mkono vuguvugu. Maandamano ya amani huhakikisha kila mmoja anashiriki (tofauti na wanaume walioshiba kwenye kudai haki kwa mtutu wa bunduki) na kudai haki kwa njia ya amani huwa na uwezekano mkubwa wa kuungwa mkono na jamii nzima.

**5. Ongezeko la watu kupuuza maagizo kutoka juu**

Moja ya nyenzo kubwa za mtawala ni uwezo wa kutumia mbinu ya kukamata kamata raia, na mavuguvugu makini huwa yanajifunza namna ya kupunguza athari za kamatakamata wakati huo huo yakiongeza ugumu wa kufanikisha hilo. Njia mojawapo wanatumia ni kupitia tathmini ya kina kuhusu madhara na uchaguzi wa mbinu inayofaa kwakuwa mbinu zote hutofautiana kwenye kupunguza kamatakamata. Wakati upambanaji wa pamoja kwa mfano maandamano makubwa kwa kiasi kikubwa huambatana na kamatakamata, mbinu za wananchi wa kawaida kama vile kususia kununua bidhaa fulani, migomo ya kukaa majumbani, kugoma kwenda shuleni kwa kisingizio cha kuumwa, au vitendo vingine vidogo vidogo visivyo vya wazi sana kwenye maeneo ya umma yanayoipa dola changamoto zaidi katika kutumia nguvu kubwa ni kwa sababu washiriki katika baadhi ya mbinu (kwa mfano kususia kununua bidhaa



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

fulani) hazionekani kirahisi (huwezi kumgundua mtu kama anasusia bidhaa au la) au vibaraka wanaoongea lakini wanajifanya hawana taarifa (kwa mfano migomo ya kukaa nyumbani inahitaji polisi wapite kila nyumba ya mfanyakazi na washiriki wanaojisingizia kuumwa wanaweza kusingizia wako hoi siku hiyo).

Mwaka 1983 nchini Chile, wapinzani wa kisiasa waliugomea udikteta wa Augusto Pinochet wakaamua kukabiliana na matumizi yake ya mabavu. Kwa mlongo mzima kulikuwa na kamatakamata kubwa, kunyongwa hadi kufa, mateso, na watu kupotezwa na hivyo watu walikuwa wanaogopa kujikusanya na kuamua kwa pamoja litakalokuwa na liwe. Mwezi Aprili, wachimba madini ya shaba waliitisha mgomo nje ya Santiago, lakini Pinochet aliwatisha kwa umwagaji damu kwa kuwatuma wanajeshi wake waliozingira mgodi kabla ya mgomo kuanza. Pamoja na vitisho hivyo, viongozi wa wafanyakazi walisitisha mgomo na badala yake, wakaanzisha mgomo wa siku moja wa nchi nzima, ambapo kila mtu aliyekuwa kwenye mgomo alifanya kazi taratibu, alitembea taratibu, aliendesha gari taratibu, na ilipofika saa 2 usiku walipigapiga vikaangio na masufuria.[16] Kulikuwa na ushiriki wa kipekee na mkubwa sana kwenye vitendo hivi, na migomo iliendelea hadi mwezi mzima. Hii ilikuwa ni hatua ya kwanza kubwa sana ya kutupilia mbali vitisho na hivyo kusambaratisha utawala wa Pinochet. Vitendo hivi havikuwa na madhara makubwa kwa washiriki na ilikuwa ngumu kuvidhibiti— majeshi ya ulinzi ya Pinochet hayakuwa na cha kufanya kutokana na mbinu nyingi za wananchi wa kawaida.

Njia nyingine ni za kufifisha athari za matumizi ya mabavu, au kuongeza ugumu katika kukabiliana na uwezekano wa kumgeuzia kibao mtawala, kuongeza manung'uniko pasipo kuhusisha siasa (waandamanaji kuomba maji safi na ujirani mwema, tofauti na kuangusha utawala), kuandaa viongozi wa kurithi, na kuweka tofauti za kijamii kati ya washiriki wa vuguvugu na makundi ya ndani na kimataifa, ili nguvu kubwa iliyowekwa kwa ajili ya kupinga vuguvugu ilmrudie mtawala. Kwa mfano, mwandishi wa blog Mmisri Khaled Said alivyotolewa kwenye mgahawa wa internet mwaka 2010 na kupigwa na polisi hadi kupoteza maisha kwa kuonesha tuhuma za kifisadi, kundi la kipinzani la Facebook lililojiita "We are All Khaled Said" (yaani Sote Sisi ni All Khaled Said) walipambana na serikali ya Misri kwa kukatisha maisha ya Said. Kwa umoja wao, waliweka wazi kwamba Said alikuwa na mapenzi mema na Wamisri wote, na hivyo mtego wa panya ukamgeukia mtegaji.

## 6. Ongezeko la watu kupuuza maagizo kutoka juu

Kadri nguvu ya umma inavyopamba moto na kadri muda unavyoyoma, husababisha mabadiliko katika uungaji mkono na wale wanaomuunga mkono



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

mtawala ama kimya kimya au kwa vitendo huanza kupuuza maagizo yake. Kwa mfano, wataka mabadiliko na wale vichwa ngumu kwenye serikali wanaweza kuanza kupishana kauli katika udhibiti. Matakwa ya kiuchumi huanza kuishinikiza nchi kukubali matakwa ya vuguvugu ili biashara iweze kuendelea. Watendaji wakuu wa dola kama wanajeshi, polisi, viongozi, na wengineo wanaweza pia wakaanza kubadili uungaji mkono, kwakuwa tayari pengine wameshavutiwa na matakwa ya waandamanaji, wamechoshwa na dola, au kwakuwa wana wanafamilia na marafiki ambao wanashiriki katika nguvu ya umma. Hata wasomi ambao huwa wana huruma na dola wanaweza kuanza kuwa na wasiwasi na uendelevu wake na hivyo kubaki bila kushabikia upande wowote ili kuepuka kuingia katika historia ya kupata misukosuko endapo wananchi watashinda.

Nchini Ukraine, Vuguvugu la Orange (Uvumilivu) la mwaka 2004, wapinzani walitumia kwa makusudi njia za mawasiliano na vyombo vya ulinzi na usalama, utegemezi wao ukiwa kwa maafisa jeshi wastaafu kama watu wa katikati.[17] Baada ya muda, upinzani kupitia vitendo vyake ulionekana unatumia njia za amani na ulikuwa sahihi; ukaomba vyombo vya ulinzi na usalama kulinda mali za raia; ukaweka kando tofauti za kijamii kwa kujichanganya, kauli mbiu, na vitendo (kama vile kutoa mauaridi kwa polisi waliokuwa fezuli);waligundua ufisadi wa dola tawala; na hatimaye kuhamasisha vyombo vya ulinzi na usalama kukataa kitii maagizo kutoka juu. Kilipofika kipindi cha kuanza kamatakamata, wanajeshi na askari polisi wengi wa Ukraine walikuwa hawana upande wowote. Hili pia lilitokea Serbia ikiwa chini ya Milosevic. Pasipo kupuuza waziwazi maagizo kutoka juu, vyombo vya ulinzi na usalama waliamua kutotii kabisa maagizo ya dola. Kwenye kilele cha vuguvugu la Otpor mnamo tarehe 5 Oktoba, afisa polisi aliyekuwa na jukumu la kuwarushia manyunyu ya kemikali kutoka kwenye helikopta makundi ya waandamanaji waliokuwa maeneo ya Belgrade aligoma kufanya hivyo, akidai kwamba asingeweza kuwaona vyema kwani hali ya hewa ilikuwa mbaya, wakati jua lilikuwa kali tu. Baadaye alitoa tamko kwamba alishindwa kutekeleza maagizo kwa sababu alihisi familia yake nayo ilikuwa kwenye miongoni mwa waandamanaji siku hiyo.[18]

Iwe kwa kushawishiwa na wengine au kwa maamuzi binafsi, kupuuza maagizo kutoka juu kama haya mara nyingi ni matokeo ya michakato ya muda mrefu yanayokuwa yamekuzwa na vuguvugu la nguvu ya umma. Kama tulivyoona kwenye orodha mbili za mienendo, mwenendo huu unatokana na umoja thabiti wa vuguvugu, kuweka mipango na maandamano ya amani. Data zinaonesha ushiriki wa njia mbalimbali huendana na uwezekano mkubwa wa kukaidi maagizo kutoka juu, wakati umoja, kupanga mipango, na maandamano ya

© 2014 Peter Ackerman na Hardy Merriman
amani huchangia kuwepo kwa ushiriki mkubwa na wa kutumia mbinu nyingi. Kipekee, maandamano ya amani ni muhimu kwenye kusababisha watu kupuuza maagizo kutoka juu. Kwakuwa vuguvugu huendelea kuwa la amani na kuepusha kujihusisha na uasi wa kutumia nguvu (kama ilivyotokea hali ya kusikitisha nchini Syria mwaka 2011), vuguvugu la hivyo huimarika hadi kesho yake na uwezekano wa wengi kupuuza maagizo kutoka juu huongezeka. Kama walengwa kwenye kuhamisha uungaji mkono ndani ya utawala hawajapigwa mikwara na waandamanaji waasi wenye kutumia nguvu, basi kupuuza kwao maagizo kutoka juu huwa tishio kubwa kwenye muundo wa utawala dhalimu.

## Msaada kwa Mdau wa Nje

Orodha hii ya mambo kadhaa si kwamba ni mwongozo muhimu kwa wapinzani tu. Watu wengine wanaweza kuutumia pia ili kuleta ufanisi kwenye mapambano yanayohusiana na migogoro hii.

Kwa mfano, orodha ya mambo inaweza kuwasaidia waandishi wa habari kutoa kwa mapana taarifa juu ya nguvu ya umma. Kama waandishi wa habari wanataka kuingia kwenye mgogoro na kupata taarifa za kina, orodha ya mambo kadhaa ingeweza kuonesha kwamba kumweka mtoa habari mbele ya bomu la chupa kule Kiev mwanzoni mwa 2014 ili aweze kusoma alama za nyakati kama nguvu inaweza kuongezeka na kuleta madhara haileti tija katika mgogoro. Hata hivyo, upelelezi kwenye umoja na mipango ya vuguvugu, vyanzo vya makosa kwenye maandamano ya amani, kuongezeka kwa washiriki, kupungua kwa madhara yanayoweza kutokana na kamatakamata kwenye vuguvugu, na kama vyombo vya ulinzi na usalama vinatii amri kwa dhati, ukiacha wale wanaopuuza maagizo kutoka juu, inaweza kutoa taswira pana kwenye uchambuzi. Kwa kuongezea, uelewa kwenye kupoteza uungwaji mkono kutoka kwa wafanyabiashara na hapa inaonesha wazi kwanini Rais wa Ukraine Yanukovych alikimbia tarehe 21 Februari mwaka huu, saa kadhaa baada ya nguvu mbaya ya vibaraka wake kumrudi. Unaweza kubashiri kirahisi nini kitajiri kama unaangalia vema viashiria vilivyowekwa.

Watunga sera wangeweza kutumia viashiria hivi katikati ya mwaka 2011, orodha hii ingeweza kuwasaidia kuona uwezekano mkubwa wa nguvu ya umma kuweza kushinda utawala wa Assad nchini Syria. Wengi kuendelea kubadili uungaji mkono (ukiacha askari wa kisuni) kwenye jeshi na kuouuza maagizo ya ingeweza kuwapa picha ya matumaini ya ushindi. Kiashiri kingine kilikuwa wafanyabiashara kujitoa kwenye uungaji mkono kwa dola. Kwa picha hii, kuwapa motisha Jeshi Huru la Syria mwanzoni mwa 2012 kuwatimua askari



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

wachache waliobaki kumuunga mkono Assad ingeonekana mbinu ya kipinzani kujirudi kama siyo ubashiri wa maafa.

Orodha ya mambo kadhaa inaweza kuwa msaada kwenye kutengeneza kanuni za kusaidia misaada ya nje kwa ajili ya mavuguvugu ya wananchi wa ndani. Kwenye orodha yanahusiana zaidi na maarifa na yanaweza kutiwa nakshi kwa kupeana taarifa za kina. Kwa mujibu wa Ibara ya 19 ya Azimio la Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu, watawala dhalimu hawana mamlaka ya kukataza taarifa kupita mipaka ya nchi zao au kuwaadhibu raia wanaotoa hizo taarifa kwa wapinzani. Mambo yote sita kwenye orodha yanaweza kusaidia kupenyeza mawazo kwa njia ya kiteknolojia na hivyo kuboresha mambo matatu chachu na mienendo mitatu.

## Orodha na Migogoro ambayo Itabadili Maisha Yetu Yajayo

Mazingira ambamo migogoro baridi inafanyikia huwa ngumu sana kutambua, na raia wapigania haki — wenye kuhitaji ushiriki kuanzia ngazi za chini ili kutumia mbinu nyingi kwenye mkakati wa kuleta ushindi —mara nyingi hukutana na vigingi vya kutoelewana. Uoga wao wa asili wa kufanya makosa kwenye kufanya maamuzi juu ya maisha ya raia na uhuru husaidia kupunguza nguvu kitu ambacho mtawala dhalimu hupenda na hivyo kumwimarisha mtawala dhalimu kiulinzi.

Orodha ya mambo kadhaa inaweza kuwasaidia wapinzani kupambana nah ii hali ya kutoelewana na kutafuta njia ya kusonga mbele. Wengine wanaweza kusema kwamba kwa kutumia mambo mengi katika mapambano, orodha kwa ajili ya kutokomeza udhalimu inaweza kuwa nyepesi mno, na kutathmini ufanyaji maamuzi sahihi kwenye migogoro ijayo kutahitaji umakini sana wa mambo ya kipekee kipindi hicho na katika mazingira husika.

Hata hivyo, orodha ya mambo hairuhusu kupuuza mambo maalum kwenye mazingira fulani, bali kuyaelewa hayo mambo kwenye muktadha mpana wa muundo mkakati ambao unaonesha kwanini na kwa namna gani mavuguvugu ya ngivu ya umma yanaweza kufanikiwa. Atul Gawande, ambaye amegfanya utafiti juu ya umuhimu wa kuweka orodha kwenye miktadha mingine kadha wa kadha, anaandika:

> Orodha ya mambo kadhaa huweza kumtetea kila mtu, hadi wanye uzoefu, dhidi ya kushindwa kwenye mapambano kadhaa kuliko



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

> tulivyofanikisha hayo mapambano. Husaidia namna fulani ya kuzama kifikra. Hubadili mawazo mfu ya kurithi yaliyo ndani yetu—kumbukumbu hasi na umakini na kutulia kwa hali ya juu …[19]
>
> Kwenye mazingira magumu sana—pale ambapo maarifa yanayohitajika huzidi yale ya mtu awaye yote, na ghafla ndiyo hutawala … [orodha makini ya mambo kadhaa] hakikisha mambo ya ovyo lakini muhimu hayapuuzwi, na… hakikisha watu wanaongea na kuungana … ili kuweka kando tofauti na mambo yasiyotabirika wanayoyajua vema.[20]

Huenda orodha hii ya mambo kadhaa ikawa siyo kiashiria cha mwisho katika kubashiri nani atakuwa mshindi: dhalimu au raia. Hata hivyo, orodha ya mambo kadhaa inaweza kutumika kama jumuisho la viashiria makini na endelevu katika kuelewa namna raia wanaodai uhuru wanaweza kuruka vigingi vya mifumo ya watawala



Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

© 2014 Peter Ackerman na Hardy Merriman

**Kumbukumbu**

[1] Kwa kuzingatia utafiti wa Erica Chenoweth na Maria Stephan, ambao wanaainisha kampeni 105 za nguvu ya umma zenye kutumika kuleta mabadiliko ya serikali kwenye nchi na himaya duniani kote kwa kipindi kuanzia 1900 - 2006.

Chenoweth, Erica, and Maria Stephan. 2011. *Why Civil Resistance Works: The Strategic Logic of Nonviolent Conflict*. New York: Columbia University Press. p. 6

NAVCO 1.1 data available at:
http://www.du.edu/korbel/sie/research/chenow_navco_data.html

[2] Kwa kuzingatia vipindi vya mpito 67 kuelekea kwenye demokrasia vilivyochambuliwa kati ya 1972---2005 kwenye utafiti wenye kichwa cha habari *Namna Uhuru Unavyopatikana: Kutoka Nguvu ya Umma kuelekea Demokrasia Endelevu*. Waandishi wanaona kwamba:

"Uwezo wa nguvu ya umma ulikuwa ni kiini cha kupitisha vipindi vya mpito 50 kati ya 67, au zaidi ya asilimia 70 ya nchi ambamo vipindi vya mpito vilianza kama mifumo ya kidikteta iliyoshindwa na/ au serikali mpya zilizoinuka kutoka kwenye mataifa mengi yalikuwa na mgawanyiko. Kati ya nchi 50 ambamo nguvu ya umma ilitumika kama mkakati pekee (hii ni kusema kwamba, ama nchi ambamo kulikuwa na vipindi vya mpito vilivyoendeshwa na wananchi wenyewe au nchi ambamo kulikuwa na vipindi vya mpito vilivyoendeshwa na msaada mkubwa wa wananchi na washika madaraka), hakuna hata nchi moja iliyokuwa Huru. Leo [mwaka 2005], miaka baada ya vipindi vya mpito nchi 32 kati ya hizi ziko Huru, 14 ziko Huru Kiasi, na 4 tu ndo Bado haziko Huru."

Ackerman, Peter, and Adrian Karatnycky. 2005. *How Freedom is Won: From Civic Resistance to Durable Democracy*. Washington, DC: Freedom House. Pp. 6---7

[3] Marchant, Eleanor, Adrian Karatnycky, Arch Puddington, and Christopher Walter. 2008. Enabling Environments for Civic Movements and the Dynamics of Democratic Transition. Freedom House special report. July 18. p. 1

[4] *Ibid*. p. 1

[5] Chenoweth, Erica, and Maria Stephan. 2011. *Why Civil Resistance Works: The Strategic Logic of Nonviolent Conflict*. New York: Columbia University Press. p. 6

[6] *Ibid.* p. 9

[7] *Ibid.* p. 68

[8] *Ibid.* p. 62

Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

[9] Chenoweth, Erica. 2014 Trends in Civil Resistance and Authoritarian Responses. The Atlantic Council Future of Authoritarianism Project. April 15.

[10] Chenoweth, Erica, and Maria Stephan. 2011. *Why Civil Resistance Works: The Strategic Logic of Nonviolent Conflict*. New York: Columbia University Press. p. 66

[11] Thomas C. Schelling. 1968. “Some Questions on Civilian Defence,” in Adam Roberts, ed., *Civilian Resistance as a National Defence: Non---violent Action Against Aggression*. Harrisburg, PA: Stackpole Books. p. 304.

[12] Ackerman, Peter and Jack DuVall. 2000. *A Force More Powerful: A Century of Nonviolent Conflict*. London: St. Martin’s Press/Palgrave Macmillan. pp. 113---174

[13] Chenoweth, Erica, and Maria Stephan. 2011. *Why Civil Resistance Works: The Strategic Logic of Nonviolent Conflict*. New York: Columbia University Press. Pp. 30---61

[14] *Ibid.* pp. 30---61

[15] *Ibid.* pp. 46---49

[16] *A Force More Powerful*. Dir. Steve York. York Zimmerman. 2000. Film.

[17] Binnendijk, Anika Locke, and Ivan Marovic. 2006. Power and Persuasion: Nonviolent Strategies to Influence State Security Forces in Serbia (2000) and Ukraine (2004). *Communist and Post---Communist Studies* 39, no. 3 (September). pp. 411---429.

[18] Interview with Nebojsa Covic, *Vecernje Novosti*, Oct. 2, 2010.

[19] Gawande, Atul. 2009. *The Checklist Manifesto: How to Get Things Right*. New York: Picador. p. 47

[20] *Ibid.* p. 79

Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.

© 2014 Peter Ackerman na Hardy Merriman

Sura hii inapatikana kwenye kitabu hiki: Mathew Burrows and Maria J. Stephan (eds.), Is Authoritarianism Staging a Comeback?, Washington, DC: The Atlantic Council, 2015.